OFISI YA RAIS TAMISEMI

MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI

JARIDA LA HALMASHAURI

Februari 3-9, 2020

# Elimu Bure Ilivyosaidia Kuongeza Ufaulu Sino Sekondari



*Wanafunzi wa Sino Sekondari wakiwa Darasani*

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Sino Tanzania Friendship Mwalimu Riyadh Kadhi amesema kuwa **sera ya Elimu bure** imesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza kiwango cha ufaulu katika Shule za Sekondari hasa za Kata kwa kuwa Shule zinapata fedha kila mwezi zinazowarahisishia katika utendaji wa kazi ikiwemo ufanyaji wa mitihani na ununuzi wa vitendea kazi kama fotokopi Mashine.

Riyadhi amesema hayo Feb 7,2020 alipotembelewa na kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mtwara Mjini ilipofanya ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa madarasa mawili katika Shule hiyo.

***Inaendelea ukurasa wa 5***

## CCM Wilaya Yaridhishwa na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo



*Kamati ya Siasa ikikagua ujenzi wa madarasa manane Shule Ya Msingi Kwale*

Ikiwa kwenye ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Manispaa ya Mtwara-Mikindani Kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mtwara Mjini imeridhishwa na utekelezaji mzuri wa miradi ya Maendeleo na Ilani.

Akizungumza kwenye kikao cha tathmini ya ziara hiyo iliyofanyika februari 7, 2020 katika Ukumbi wa mikutano wa Manispaa Mwenyekiti wa Chama hicho Mhe. Salumu Mpilu ameipongeza timu ya Menejiment kwa kazi nzuri ya usimamizi wa miradi.

"Ninawapongeza Miradi ya leo ni mizuri asilimia 87 hata kama hujaenda shule ukiangalia tu kwa macho unaona kabisa kuwa kazi imefanyika" alisema Mpilu

Aidha Mpilu amewataka watumishi kuendeleza upendo baina yao ili kurahisisha utendaji wa kazi katika Taasisi wanayoitumika ili Ilani iweze kutekelezeka kwa urahisi.

Miradi iliyotembelewa na kamati hiyo ni pamoja na miradi ya ujenzi wa sehemu ya kupumzikia ya Mashujaa, Stendi ya Mikindani, Ujenzi wa choo cha Milumba, Ujenzi wa madarasa manane Shule ya Msingi kwale, Ujenzi wa Madarasa mawili Shule ya Sekondari ya Sino, Mradi wa maji wa Haikata pamoja na Lwelu.

# CCM Yashiriki Ujenzi wa Choo Milumba



Wajumbe wa Kamati ya siasa ya Wilaya wakishiriki katika ujenzi wa choo katika mwalo wa Milumba

Wakiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutembelea miradi mbalimbali ya Maendeleo inayotekelezwa ndani ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani, Februari 7, 2020 Kamati ya siasa ya CCM Wilaya ya Mtwara Mjini imeshiriki zoezi la ujenzi wa Choo cha Mwalo wa Mirumba kilichopo Kata ya Jangwani.

Choo cha hicho kinachojengwa kwa kutumia mapato ya ndani kinatajaria kutumia fedha kiasi cha Shilingi Milioni kumi hadi kukamilika kwake na kitakuwa na vyumba vitano vikiwemo viwili vitakavyotumiwa na wanawake, viwili wanaume na kimoja ni kwa ajili ya Walemavu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mtwara Mjini Salumu Mpilu amesema kuwa amefurahi kuona agizo lake alilolitoa kwa Mkurugenzi mwaka jana alipotembelea soko hilo kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa choo katika soko hilo limetekelezeka na kupongeza Ofisi ya Mkurugenzi kwa kuwajali wananchi.

Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Mhe.Geofrey Mwanichisye amewataka Wananchi kutoa nguvu zao na kujitolea pale inapobidi ili kuunga mkono juhudi za kuleta maendeleo katika nchi yao.

# Shirika la EDUCAID Lakabidhi Matundu ya Vyoo Mkangala



*Afisa Elimu  Msingi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Bi. Flora Aloys akikagua matundu ya vyoo mara baada ya kukabidhiwa kwa Shule ya Msingi Mkangala*

Katika kuunga mkono Kampeni ya Shule ni Choo iliyoanzishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Gelasius Byakanwa ,Shirika linalosaidia Elimu (Educaid Tanzania) limejenga choo na kukabidhi kwa uongozi wa Shule ya Msingi ya Mkangala iliyopo Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Choo hiko chenye matundu sita na chumba kimoja cha kujihifadhi kwa wanafunzi wasichana kitatumiwa na wanafunzi wasichana tu.

Akizungumza wakati wa kukabidhi choo hiko Februari 6,2020 Meneja wa Shirika la EDUCAID bwana Ali Said Simba amesema kuwa kwa kutambua juhudi zinazofanywa na Mkuu wa Mkoa wameona si vema wakanyamaza kimya kama wadau wa Elimu  wakaamua kujenga choo katika Shule hiyo.

Pamoja na ujenzi wa matundu ya vyoo pia Simba ameahidi kutoboa maji na kuweka miundombinu yake kwa ajili ya matumizi ya Shule h pamoja na choo hiko.

Kwa Afrika Shirika la EDUCAID linafanya kazi katika nchi ya Tanzania pekee kwa katika Mkoa wa Mtwara kwa halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani na halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Aidha Jumla ya Kata tisa zenye Shule ishirini zinafanya kazi na Shirika hilo.

*Inatoka ukurasa wa kwanza…………..*

Amesema kuwa Shule ya Sino imekuwa ikifanya vizuri katika matokeo ya Mitihani ya Kitaifa ya kidato cha nne mwaka jana imetoa mwanafunzi aliyepata daraja la kwanza pointi nane akiwa ni mwanafunzi wa tatu kuongoza kiufaulu katika Mkoa wa Mtwara akitanguliwa na wanafunzi wawili waliopata daraja la kwanza pointi saba kutoka Shule ya Sekondari ya Mtwara Ufundi na Abbey.

Aidha Riyadhi ameongeza kuwa wao kama walimu wa Shule ya Sekondari ya Sino wamekusudia kuifanya Shule hiyo kuwa Kituo cha Elimu kwa Kata ya Ufukoni na Mtwara kwa kufaulisha wanafunzi wengi zaidi na kuondoa sifuri ili kuondoa dhana dhaifu na mtazamo finyu wa wananchi kuhusu Shule za Kata.

"Kwa mwaka huu tunao wanafunzi 110 wanaotarajia kufanya Mtihani wa Kidato cha nne malengo ni kuhakikisha Zaidi ya wanafunzi hamsini na tano wataenda kidato cha tano na waliobakia waende katika vyuo vya Maendeleo ,Kilimo na



Madarasa Shule ya Sekondari ya Sino

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mstahiki Meya wa Manispaa Geofrey Mwanichisye akishiriki katika ujenzi wa Choo cha Mwalo wa Milumba



Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa Grayson Orcado akishiriki katika ujenzi wa choo katika mwalo wa Milumba



Bwana Emanuel Sanga (Aliyevaa Fulana ya Bluu na weupe) akikabidhi matundu ya vyoo kwa Bwana Salumu Masalanga aliyemwakilisha Afisa Elimu Mkoa



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mtwara Mjini Mhe. Salum Mpilu (aliyevaa kofia) akisalimiana na wanafunzi wa darasa la saba Shule ya Msingi ya Kwale



kamati ya Siasa na wataalamu wa Manispaa wakikagua mradi wa Maji uliopo Haikata Mtonya